*Journal of Linguistics and Language in Education Volume 15, Number 1 (2021)*

# Mwingiliano wa Vishazi Tegemezi na Vishazi Bebwa

*Amani J. Chipalo*[*]

**Ikisiri**

*Makala haya yanachunguza dhana za vishazi tegemezi na vishazi bebwa kutokana na matumizi tofauti ya dhana hizo miongoni mwa wanasarufi. Kuna kundi linaloona kwamba dhana hizo hazina tofauti kimaudhuibali kiistilahi tu. Aidha, inaelezwazaidi kwamba dhana ya kishazi tegemezi ina usuli wa sarufi mapokeo; yaani imeegemea kwenye semantiki zaidi kufafanua masuala ya kimuundo. Kwa msingi huo, ili kutoegemea zaidi kwenye semantiki na kuakisi umuundo katika istilahi za kisintaksia kuelezea kitu kilekile; kundi lingine linaona dhana muafaka ni vishazi bebwa. Kwamba kishazi tegemezi ni sawa na kishazi bebwa kwa sababu ukamilifu wake wa maana unategemea kishazi huru na kimuundo kinakuwa kimebebwa ndani ya muundo wa kishazi huru. Hivyo, kwa mtazamo wa kundi hili; dhana hizo ni visawe na yoyote kati yake inaweza kutumika badala ya nyingine. Lakini kundi lingine linaziona dhana hizo kuwa tofauti na kamwe haziwezi kuwa visawe. Sababu kubwa ni kwamba dhana hizo hazina usawe wa namna yoyote kwani kinyume cha kishazi bebwa ni kishazi sibebwa. Kama zingekuwa sawa, ingetazamiwa kwa mtazamo huu kuwe na vishazi bebwa na sibebwa lakini haiko hivyo. Kutokana natofauti hiyo ya mitazamo, makala haya yametumia data za lugha ya Kiswahili kubaini mwingiliano na tofauti iliyopo kati ya dhana ya kishazi tegemezi na kishazi bebwa. Data zilikusanywa kutoka kwenye mifano[18]ya darasani namachapisho mbalimbali yaliyokwishafanya uchunguzi au ufafanuzi kuhusu vishazi na sentensi za lugha ya Kiswahili. Pia, data hizo zilichanganuliwa kwa mwega waNadharia Rasmi Panufu. Matokeo yanaonesha kuwa kishazi tegemezi kina sifa ya ama kutumia viambishi vya urejeshi kwenye kitenzi au kudokezwa kwa kiunganishi tegemezi kinachoweza kuwa bayana au kisiwe bayana. Vilevile, uchambuzi wa data umeonesha kuwa kishazi bebwa chenyewe hubainika kimuktadha. Kimsingi, huwa ni kishazi tegemezi ambacho katika muundo wa sentensi hakiwezi kuondolewa bila kuathiri uarifu wa kitenzi au nomino katika kishazi hurucha sentensi husika. Sifa na tabia za vitenzi na nomino za lugha ya Kiswahili kisemantiki na kisintaksia ndiyo huamua ubebwa wa vishazi tegemezi. Kwa hiyo, makala yanahitimisha kuwadhana hizo haziwezi kutumiwa kama visawe ingawa kunamwingiliano kati yake. Kishazi tegemezi ni aina mojawapo katika mgawanyo wa aina kuu za vishazi ilhali kishazi bebwa ni aina mojawapo ya vishazi tegemezi. Kwa kifupi, kulingana na muundo wa sentensi kishazi tegemezi kinaweza kuwa bebwa au sibebwa.*

**Dhana za msingi:** *vishazi bebwa, vishazi tegemezi, kanuni ya ujirani*

[*]Assistant Lecturer, Department of Languages and Literature, Dar es Salaam University College of Education, P.O. Box 2329, Dar es Salaam, Tanzania, E-mail: amanichipalo4@gmail.com

[18] Baadhi ya data zilizotumika katika makala haya zilitokana na mifano *wakati wa* mihadhara ya kozi ya Sintaksia kwenye muhula wa pili wa darasa la PhD (Kiswahili) kwa tamrini na tasinifu mwaka 2019/2020. Namshukuru muhadhiri wetu Dkt. Luinasia Kombe namwanafunzi mwenzangu Abdallah Ibrahimu.

**Abstract**

*This study explores the subordinate and embedded clause concepts following their differences in usage among grammarians. There are grammarians with an approach that the terms have no difference content in description but only terminological difference. Also, it is further explained that the concept of subordinate clause has a background in traditional grammar; that is, it is more semantic in describing syntactic issues. With that basis, in order to avoid relying on semantics as well as reflecting syntactical flavour in terminologies; there is an approach purporting to use embedded clause instead of subordinate clause. The subordinate clause is synonymous to embedded clause because they all make sense when attached to an independent clause. Therefore, this approach considers the terms synonyms and they can be used interchangeably. But there is another approach which does not take these concepts as synonyms. The only reason is that the terms are no how related and they cannot be used interchangeably since the opposite of embedded clause is unembedded clause, not subordinate clause. Due to such difference in approach, this study uses Kiswahili data to find out the connection and difference existing between these two terms, subordinate and embedded clauses. The data were gathered from examples used during lectures in a PhD (Kiswahili) class and various publications that had explored about clauses and sentences in Kiswahili. Moreover, those data were analysed based on the Extended Standard Theory. The findings revealed that subordinate clauses are characterised by two main features: the presence of reflexive affixes in a verb or the use of subordinators which can be overt or covert. On the side of embedded clauses, the findings showed that it is contextually identified. Generally speaking an embedded clause is a subordinate clause which cannot be omitted in a sentence without distracting the predication of the verb or noun in the independent clause of matrix sentence. The semantic and syntactic features of the Kiswahili nouns and verbs dictate the embedment of the subordinate clauses. It is thus concluded that these terms cannot be used synonymously. Nevertheless, the terms are related since the subordinateclause is one of the main types of clauses while the embedded clause is one among the types of subordinate clauses. Simply put, depending on the structure of a sentence the subordinate clause can either be embedded or unembedded.*

## Utangulizi

Kishazi ni darajia mojawapo ya tungo katika uainishaji wake(Massamba, Kihore, na Hokororo, 1999). Kwa hiyo, ni wazi kuwa kishazi ni mojawapo ya kategoria za kisintaksia katika udarajia wa tungo. Pamoja na kutamkwa kwake kama mojawapo ya vijenzi vya tungo, bado kuna changamoto za kidhana na kiuainishaji, hususani katika lugha ya Kiswahili. Kwa kifupi, kumekuwa na mawazo kinzani kuhusiana na dhana ya kishazi katika fasili na uainishaji wake.

Kuhusu fasili ya kishazi,Wesana-Chomi (2017) anadai kuwa ni kiambajengo cha kisintaksia kinachoundwa na kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Fasili hii imeegemezwa katika viambajengo vinavyounda kishazi. Hata hivyo, uambajengo katika sintaksia haubainishwi kwakutaja vijenzi vyake tu. Mkude (1983) aliwahi kueleza kuwa 'ukubwa au udogo' wa kiambajengo 'hautegemei upana wala urefu' kwa maana na idadi ya vijenzi vya kiambajengo husika. Vilevile, kwa kuzingatia tabia ya lugha kimofolojia baadhi ya viambajengo huweza kubebwa na viambishi tu katika kiambajengo kingine (taz. Stockwell, 1977). Bila shaka kwa kutambua suala hili ndiyo maana hata Wesana-Chomi mwenyewe bado anaeleza kuwa kishazi kinaweza kuundwa na kiambajengo kimoja. Hii ina maana kuwa si lazima kishazi kuwa na kirai nomino na kirai kitenzi. Kama Massamba na wenzake (1999) wanavyoeleza, kishazi kinaweza kuundwa na kirai kitenzi peke yake.

Kwa upande wao, Massamba na wenzake (1999) wanaeleza kuwa kishazi ni tungo yenye muundo wa kiima kiarifu. Inaelezwa zaidi kuwa kitenzi ni kiambajengo cha lazima katika muundo wa kishazi kwani ndicho huwa na dhima ya uarifishaji. Aidha, kitenzi kama kiini cha uarifishaji ndicho huamua na/au kuchagua viambajengo vya kukikumusha au kuandamana nacho (Tallerman, 2011). Kama ilivyokuwa kwa fasili ya awali, fasili hii pia ina dosari; kwa mfano, madai kuwa kishazi kina muundo wa kiima kiarifu hayakitofautishi na kirai kitenzi na sentensi. Vilevile, sentensi mbali na kuwa na muundo wa kiima kiarifu pia kiini chake ni kitenzi. Kwa hali hii, siyo rahisi kutofautisha kishazina sentensikwa kwa kutumia fasili peke yake.

Kwa upande wa uainishaji wa vishazi, kumekuwa na mawazo kinzani yanayoweza kuwekwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza linagawa vishazi katika makundi mawili ya vishazi huru na vishazi tegemezi (taz. Habwe na Karanja, 2004; Payne, 2006; Tallerman, 2011). Kadhalika,Massamba na wenzake (1999)wanaunga mkono wazo la kuainisha vishazi katika makundi mawili lakini wao wanatumia istilahi ya vishazi-viambatani kumaanishavishazi huru, na kuikubaliile ya vishazi tegemezi. Aidha,Wesana-Chomi (2017)anakubaliana na kuainisha vishazi katika aina mbili lakini yeye anatumia istilahi za vishazi vikuu na vishazi bebwa.

Pia, Tallerman (2011) anaunga mkono madai ya ubebwa wa vishazi kwa kusema kuwa vishazi tegemezi huwa vimebebwa katika muundo wa sentensi kuu. Kwa maneno mengine, kauli hiyo inaelekea kukubaliana na uainishaji unaozichukulia dhana za vishazi tegemezi na vishazi bebwa kama visawe. Hata hivyo, kuna madai kwamba baadhi ya wanasarufi wameendeleza istilahi za kimapokeo. Kwa mfano, Wesana-Chomi (2017) anaeleza kuwa kishazi tegemezi ni dhana ya kwanza kutumika wakati wa Sarufi Mapokeo ambapo baadaye katika Sarufi Zalishi dhana hiyo imeonekana kutokidhi haja za kisintaksia na hivyo kupendekezwa kwa matumizi ya istilahi ya kishazi bebwa. Kwa maneno mengine, dhana za kishazi tegemezi na kishazi bebwa zinachukuliwa kama visawe. Makala haya kwa mwega waa Nadharia Rasmi Panufu; yanatumia data za lugha ya Kiswahili ili kubaini mwingiliano wa dhana za utegemezi na ubebwa wa vishazi, yaani kama dhana ya kishazi bebwa ni sawa na kishazi tegemezi au ni tofauti isipokuwa zinaingiliana.

**Uainishaji wa Vishazi katika Kiswahili**

Tumekwishaona kuwa vishazi huweza kugawanywa katika sehemu mbili. Pamoja na mgawanyo huo, bado kuna matumizi ya istilahi tofauti kurejelea aina hizo. Rauh (2010) anatahadharisha matumizi ya istilahi zaidi ya moja kurejelea kitu hichohicho kwani yanaweza kupotosha msomaji au kuleta tofauti kutokana na misingi ya nadharia iliyotumika kuunda istilahi hizo. Mathalani, katika lugha ya Kiswahili kuna wanaotumia istilahi ya 'kishazi tegemezi'ilhaliwengine wakitumia 'kishazi bebwa' badala ya kishazi tegemezi. Sehemu hii inapitia mawazo na ufafanuziwa wanasarufi wa mitazamo yote ili kutathmini na kubaini kama kuna mwachano au mwingiliano katika matumizi ya istilahi hizo.

Massamba na wenzake (1999)ni miongoni mwa wanaotumia istilahi ya vishazi tegemezi na wanafafanua kuwa ni vile vishazi visivyoweza kusimama peke yake vikiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu. Madai haya yanaungwa mkono na wanasarufi wengine kama vile Borsley (1999), Robins (2013), na Tallerman (2011) tukiwataja kwa uchache. Fasili ya namna hii inajengwa katika misingi ya kimaana na kimuundo kama sababu za kufanya kishazi kisiweze kusimama peke yake na kujitosheleza na hivyo kuwa tegemezi. Katika namna sawa ya kuonesha utegemezi wa vishazi, Payne (2006) anaeleza moja ya sababu kuwa uambishaji wa njeo hufanyika katika kitenzi cha sentensi kuu. Hata hivyo, hii haina

maana kuwa vitenzi katika vishazi tegemezi huwa havina viambishi vya njeo. Kitenzi katika kishazi tegemezi kinaweza kuwa nakiambishi cha njeo na utegemezi wake ukadokezwa kwa namna nyingine.

Kama anavyoeleza Robins (2013), utegemezi wa vishazi huoneshwa kwa namna mbalimbali kutegemeana na lugha. Kwa mfano, katika lugha ya Kiswahili utegemezi wa kishazi upo wa namna mbili: matumizi ya viambishi vya urejeshi naviunganishi tegemezi (Massamba na wenzake, 1999; Mekacha, 1987; Mpiranya, 2015; Polomé, 1967). Kwa kutumia viambishi vya urejeshi kitenzi cha kishazi tegemezi husika huwa na kiambishi cha o- rejeshi kurejelea nomino iliyo katika kiima. Kwa mfano:

(1) (a) *Mtoto ali**ye**kuja jana* ameondoka.
(b) Mwalimu amewaadhibu *wanafunzi wali**o**piga kelele.*
(Chanzo: Mekacha, 1987:86)
(c) *Mayaiuli**yo**nunu*a ni mabovu.
(d) *Saauli**yo**mpa* imevunjika.
(Chanzo: Polomé, 1967:161)

Mifano hiyo hapo juu kwenye data (1) inaonesha vishazi tegemezi vikiwa katika hatimlalona vitenzi vyake vina kiambishi cha urejeshi kilichokolezwa wino.Kiambishi hicho ndicho hukipa kishazi husika hadhi ya utegemezi. Vilevile, kiambishi cha urejeshi kinaweza kuambikwa kwenye mzizi amba- na hivyo kuwa kishazi tegemezi kinachodokezwa na amba- kama mifano katika data (2a-c) inavyoonesha.

(2) (a) *Watotoamba**o**wanapenda kusoma* watafaulu.
(b) *Nyumba amba**yo** paa lake limeharibika……*
(c) Ninajua *nchi amba**yo** mshiriki wakeameshinda.*
(Chanzo: Mpiranya, 2015:72)

Kwa upandewa vishazi tegemezi ambavyo hudokezwa kwa viunganishi tegemezi,utegemezi wake husababishwa na viunganishi hivyo. Massamba na wenzake (1999:131) wanaviita viunganishi hivi 'maneno maalumu'. Katika Kiswahili kuna viunganishi tegemezi kama vile *kuwa, ingawa, kwamba, ili, iwapo, kama* na vingine vingi (taz. Wesana-Chomi, 1973). Viunganishi hivi vinapokitangulia kishazi hukitweza na kukikosesha sifa ya kuweza kusimama peke yake na hivyo kuwa kishazi tegemezi. Kwa mfano:

(3) (a) ***Kama*** *atasafiri* nitamsindikiza.
(b) ***Japokuwa*** *mnanisakama* sitaacha kufanya kazi.
(c) ***Ili*** *nilale* nahitaji vidonge.
(Chanzo: Massamba na wenzake, 1999:131)

Mifano iliyotolewa hapo juu katika data (3) ni ya vishazi tegemezi vilivyodokezwa kwa viunganishi tegemezi vilivyokozwa wino. Aidha, kama anavyosema Kombe (2018), mara nyingi tungo husikika kwa muundo wa nje baada ya kupitia hatua mbalimbali za mageuzi. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa kuwa na kishazi tegemezi kisichokuwa na kiunganishi tegemezi bayana. Kwa mfano:
(4) (a) Watoto wanasema (*kuwa) nyumba inaungua.*
(Chanzo: Mkude, 1983:242)
(b) Baba aliwakataza watoto *(kuwa) wasiingie katika zizi la nguruwe.*
(c) Ahmed na Fatuma walienda mjini *(ili) waone senema.*
(d) Juma alimwambia Ahmed (*kwamba) Hamisi anakuja.*
(Chanzo: Vitale, 1981:65)

Mifano iliyo kwenye data (4) hapo juu inaonesha vishazi tegemezi katika hatimlalovikiwa na kiunganishi tegemezi kwenye mabano. Kimsingi, mabano yanaashiria uziada au uhiari uliopo kwenye matumizi ya viunganishi hivyo. Maana yake ni kwamba kuwepo au kutokuwepo kwa viunganishi hivyo hakuathiri usarufi wa tungo husika. Kuwepo au kutokuwepo kwa viunganishi hivyo hutegemea mageuzi yatakayokuwa yamefanyika katika tungo husika kama anavyoeleza Kombe (2018). Kwa hiyo, kuna uwezekano wa kishazi tegemezi kutokuwa na kiunganishi tegemezi cha wazi.


Kwa upande wa wale wanaotumia dhana ya kishazi bebwa, hoja kubwa ni kutaka kutenganisha au kuweka mipaka baina ya tanzu za sarufi. Wenye mtazamo wa kutumia dhana ya kishazi bebwa badala ya kishazi tegemezi wanataka kuachana na uanamapokeo ambao wanadai uliegemea kwenye semantiki zaidi. Kwa hiyo, wanadai kwamba kwa kuwa kishazi ni dhana ya kisintaksia ni vema ikafasiliwa kisintaksia; siyo kisemantiki kama ilivyokuwa hapo awali (Wesana-Chomi, 2017).

Mapitio ya ufafanuzi wa pande hizi mbili (unaotumia istilahi kishazi tegemezi na ule unaotumia kishazi bebwa)yamedhihirisha kwamba mbali na istilahi hakunatofauti ya sifa wala muundo kati yakishazi tegemezi na kishazi bebwa. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa na Rauh

(2010), sarufi mapokeo haikujikita katika utafiti na uchambuzi wa data za lugha mahsusi kabla ya kufanya hitimisho. Kwa hiyo, hata dhana zilizokuwa zinaundwa hazikuakisi uhalisia. Hivi ni kusema kwamba nadharia zilizofuata baada ya sarufi mapokeo zimekuwa na kazi ya kuunda istilahi mpya kama ambavyo istilahi ya kishazi bebwa inapendekezwa na Wesana-Chomi (2017) kutumiwa badala ya kishazi tegemezi.

**Mwega wa Kinadharia**

Uchambuzi wa data katika makala haya umeongozwa na Nadharia Rasmi Panufu(kuanzia sasa NRP).Kwa mujibu wa Rauh (2010) NRPni matokeo ya maboresho ya Chomsky (1973) katika hatua ya pili ya maendeleo ya Nadharia ya Sarufi Zalishi. Kabla ya kuibuka kwa NRP, Chomsky alikuwa amependekeza uchanganuzi wa sentensi kufanyika kwa misingi ya Nadharia Rasmi. Hata hivyo, uchanganuzi huo ulikumbwa na changamoto ya mageuzi kubadili maana ya msingi ya sentensi husika. Kwa hiyo, lengo la kuanzisha NRP lilikuwa kuzuia mageuzi yasibadili maana.Mageuzi yalidhibitiwa zaidi ili yasibadili maana kwa kuongeza kitengo cha msingi katika ufafanuzi wa nadharia hii. Ufanyaji kazi wa nadharia hii unaweza kufupishwa kwa mchoro kama ifuatavyo.




Kielelezo 1: Muhtasari wa kiunzi cha Nadharia Rasmi Panufu

(Chanzo: Rauh, 2010:64)

Kielelezo Na. 1 kinaonesha kwa ufupi jinsiNRPinavyofanya kazi. Kielelezo kinaonesha kuwa uelewekaji wa sentensi yoyote huhusisha kitengo cha msingi ambacho kina msamiati wa lugha husika na kanuni za muundo virai ambazo huongoza uambajengo katika lugha hiyo. Kwa hiyo msamiati huo na kanuni zake huunda muundo ndani ambao huonesha jinsi msamiati huo uanvyotakiwa kupangwa kuunda viambajengo. Tofauti na ilivyokuwa katika nadharia za

mwanzo, katika NRPkinaongezwa kitengo cha ufasili wa maana (semantiki) ili kuupatia maana ya msingi muundo ndani (Chomsky, 2015).

Aidha, kutegemeana na mahitaji ya wazungumzaji wa lugha, muundo ndani huweza kugeuzwageuzwa kwa namna mbalimbali ili kukamilisha haja ya mawasiliano. Kwa hiyo kama kielelezo kinavyooneshwa muundo ndani wenye maana yake ya msingi huingizwa kwenye kanuni za mageuzi ya ama kudondosha, kuhamisha au kuongeza viambajengo ili kukamilisha haja ya mawasiliano.Baada ya mageuzi sentensi katika muundo wa nje hiyo hupata sura au umbo la kutamkika kupitia kitengo cha ufasili wa kifonolojia.

Pia, Rauh (2010) anaeleza zaidi kwamba katika NRPkitengo cha mageuzi kilidhibitiwa zaidi kwani endapo kiambajengo kilihamishwa ilibidi kiache nyayo.Hivi ni kusema kuwa wakati huu NRPilizipa nafasi fonolojia, sintaksia na semantiki. Hali hiyo ilisababisha kuzalisha miundo ya nje ya sentensi mbili iliyodhaniwa kuwa na maana moja ilhali ilikuwa na maana tofauti kwa sababu zilikuwa tofauti katika muundo wa ndani.

Kwa kuwa shabaha yake ilikuwa kuzalisha miundo inayokubalika katika lugha,Chomsky (2015) anasisitiza kuwa mfumo wa kanuni za kuzalisha miundo hiyo katika NRP sharti uchanganuliwe katika vipengle vitatu: sintaksia, fonolojia na semantiki kama kielelezo Na. 1 kinavyoonesha. Kwa kuongeza kitengo cha ufasili wa maana, katika NRM kipengele cha sintaksia kinajumuisha miundo yote yenye taarifa zinazowezesha upatikanaji wa fasili moja kwa kila sentensi. Kwa maneno mengine, haikutarajiwa miundo hiyo kutoeleweka au kuchanuza utata. Kipengele cha fonolojia kwa upande wake, kilishughulika na umbo la kifonetiki la sentensi iliyozalishwa na kanuni za kimuundo katika kipengele cha sintaksia. Kwa kifupi, kipengele cha fonolojia kilishughulika na masuala ya kimatamshi kwa sentensi zilizozalishwa. Vilevile, kipengele cha semantiki kwa upande wake kilishughulika na fasili ya tungo zilizozalishwa na kanuni za kimuundo katika kipengele cha kwanza.

Kwa hakika kiunzi hiki kinafaa kuongoza uchanganuzi wa data za makala haya. Kama tulivyoeleza katika utangulizi wa makala, lengo ni kuchunguza uanishaji na matumizi ya dhana ya kishazi tegemezi na kishazi bebwa. Aidha, ilielezwa kuwa dhana ya kishazi tegemezi

ina msingi katika sarufi mapokeo ambayo iliegemea zaidi katika semantiki. Kishazi bebwa kwa upande wake tuliona kuwa ni dhana iliyo na msingi katika sintaksia. Tuliona kuwa muundo na ukamilifu wa maana katika kishazi tegemezi umetegemezwa kwenye kishazi kikuu cha sentensi husika. Kwa hiyo, kwa kuwa NRP inaweka pamoja semantiki na sintaksia, inatarajiwa nadharia hii kuwa faafu kuongoza uchambuzi wa data za makala haya.

Kadhalika, kama istilahi kishazi bebwa inadaiwa kuwa kisawe cha kishazi tegemezi (Wesana-Chomi, 2017), tunatarajia kuona kishazi hicho kuwa kimebebwa ndani ya muundo na utoshelevu wa maana wa kishazi kikuu. Kwa hiyo, katika muktadha huu, uchanganuzi wa data utazingatia zaidi vipengele vya sintaksia na semantiki. Hii ina maana kuwa vipengele vya muundo ndani, muundo nje na kitengo cha ufasili wa kifonolojia havitahusishwa katika uchambuzi wa data.

Uamuzi wa kutumia vipengele vya sintaksia na semantiki unatokana na ufafanuzi wa Chomsky (2015) kuwa maana ya sentensi hutokana na maana ya viambajengo vya sentensi husika. Hii ina maana kuwa maneno katika lugha huwa na sifa tofauti za kisintaksia na kisemantiki.Kwa mfano,Tallerman (2011) anaeleza kuwa katika Kiingereza vishazi tegemezi huunda elementi za lazima katika sentensi. Ikumbukwe pia tumesema kwamba utegemezi wa kishazi huamuliwa na kitenzi kikuu cha sentensi. Kwa hiyo, tabia za kisintaksia za vitenzi ndizo zitaonesha kama kitenzi husika kinahitaji kujalizwa na kiambajengo kingine ili kukamilisha muundo na maana yake au la.

Payne (2006), mbali na kuainisha dhima za kisemantiki za vitenzi katika tungo, anabainisha kuwa vitenzi kisintaksia vinaweza kuwekwa katika makundi mawili: vitenzi elekezi na sielekezi. Vitenzi elekezi huhitaji kijalizo cha lazima kukamilisha uarifu wake katika tungo wakati vitenzi sielekezi havihitaji ujalizaji wa namna yoyote ili kukamilisha uarifu wake. Kwa hiyo, inatarajiwa vipengele vya sintaksia na semantiki vitatusaidia kubaini utegemezi na/au ubebwa wa vishazi na hivyo kuweza kuhitimisha kama vishazi tegemezi ndiyo vishazi bebwa au ni dhana mbili tofauti zenye kuingiliana.

**Utegemezi na Ubebwa wa Vishazi katika Sentensi za Kiswahili**

Uchambuzi wa data unaonesha kuwa kuna uwezekano wa sentensi za Kiswahili kuwa na vishazi viwili au zaidi. Sentensi zenye uwezekano wa kuwa na vishazi viwili ni sentensi changamani na sentensi ambatani (taz. Massamba na wenzake, 1999; Mkude, 1983; Wesana-Chomi, 2017). Kwa ujumla, ufafanuzi wa aina hizo za sentensi (hasa dhana ya sentensi changamani) unatofautiana kati ya mwanasarufi mmoja na mwingine. Kuna wanasarufi wanaoainisha sentensi changamani kuwa zile zenye vishazi viwili katika muundo wake bila kujali hadhi za vishazi hivyo ndani ya sentensi (Mkude, 1983; Wesana-Chomi, 2017). Lakini kuna wanasarufi wanaoainisha sentensi changamani kuwa zile zenye kishazi tegemezi kimoja au zaidi na kishazi huru kimoja tu (Massamba na wenzake, 1999).

Pamoja na tofauti hizo kuhusiana na sentensi changamani, uchambuzi wa data za makala haya ulijikita kwenye zile sentensi zinazokuwa na vishazi viwili au zaidi vya hadhi tofauti. Hapa tunazungumziasentensi inayokuwa na kishazi huru au kikuu kimoja na kishazi kingine au vingine ambavyo kuwepo kwake kunahalalishwa au kunatokana na kishazi kikuu/huru. Kwa hiyo, kwa kutumia Nadharia Rasmi Panufu (Chomsky, 2015), uchanganuzi umefanyika kuona kama kishazi tegemezi ni sawa na kishazi bebwa. Itakumbukwa kuwa Nadharia Rasmi Panufu inaamini kuwa kila neno lina tabia zake kisintaksia na kisemantiki. Kwa hiyo, tathmini ilifanyika kuona mawanda ya matumizi ya dhana kishazi tegemezi na kishazi bebwa.

Uchambuzi wa data unaonesha kuwa vishazi tegemezi katika lugha ya Kiswahili vinafanya kazi mbalimbali za kujaliza nomino au viwakilishi, vitenzi na vihusishi. Tuchunguze mifano ifuatayo katika (5) hapa chini.


(5) (a) Juma anajua mambo mengi *ingawa hakusoma sana*
(b) Watoto *wanaolia sana* wanasema *kuwa nyumba inaungua*
(c) Mama alikwenda *alikokuwa amepangiwa*
(d) Sisi tumepata habari *kwamba mji umo katika ghasia*

(Chanzo: Mifano ya darasani)

Mifano yote iliyotolewa katika data (5) hapo juu ina vishazi tegemezi. Hata hivyo, vishazi tegemezi hivyo vina uhusiano tofautitofauti na vitenzi vikuu vya sentensi husika. Kuna vishazi

tegemezi ambavyo vinahusiana moja kwa moja na vishazi vikuu na vingine uhusiano wake na vishazi vikuu unapitia kwenye viambajengo vingine. Kwa maneno mengine, vipo vishazi tegemezi ambavyo vimebebwa na vishazi vikuu na vingine ni vishazi tegemezi lakini havijabebwa na vishazi vikuu. Tunasema kishazi tegemezi kimebebwa na kishazi kikuu ikiwa kishazi hicho ni lazima kiwepo ili kukamilisha muundo na maana ya kishazi kikuu. Aidha, kama uambajengo wa kishazi tegemezi si wa lazima kukamilisha muundo na maana ya kishazi kikuu basi kishazi tegemezi hicho hakijabebwa katika sentensi husika.

Kwa hiyo, hata uambajengo wa vishazi hivyo kwenye mchoroti utakuwa tofauti kati ya kile kilichobebwa na kisichobebwa. Inatazamiwa kuwa kiambajengo kinachobebwa kitakuwa jirani na kile kinachokibeba na kisichobebwa kitakuwa mbali na wala kutokuwepo kwake hakuathiri usarufi wa tungo husika. Kanuni ya ujirani katika muundo wa tungo inaeleza kuwa 'viambajengo vyenye ufanano wa kisemantiki huwekwa pamoja kisintaksia' (Stockwell, 1977:68). Kwa hiyo, inategemewa kuwa kiambajengo kinachobebwa na kitenzi kitakuwa sehemu ya vijenzi vya uarifu wake na kile kisichobebwa nacho kitakuwa nje ya uarifu wa kitenzi hicho. Tuangalie mifano ifuatayo ya uchanganuzi[19]:





Kielelezo Na.2: Kishazi tegemezi kisichobebwa na kishazi kikuu

[19]S kwa vifundo vya viambajengo vilivyo chini ya KN au KT katika kielelezo tungo ni vishazi au sentensi zilizoshushwa hadhi katika uambajengo wa sentensi kuu. Vilevile Ø inasimama badala ya kategoria dhahania ambazo hazina maumbo dhahiri baada ya kudondoshwa kutokana na hatua mbalimbali za mageuzi ya muundo ndani wa sentensi husika.

Kama inavyoonekana katika kielelezo Na.2, kiambajengo $S_2$ ni kishazi tegemezi kwa kuwa ni sehemu ya vijenzi vya $KN_2$. Kwa kuwa $S_2$ ni kiambajengo cha $KN_2$, basi hakibebwi moja kwa moja na kishazi kikuu "Juma anajua mambo mengi". Stockwell (1977) anaeleza kuwa viambajengo vyenye ubebano thabiti kisemantiki haviruhusu kiambajengo chochote kusimama katikati yake. Katika uchanganuzi wa kielelezo Na. (2) uliooneshwa hapo juu, inaonekana kuwa kishazi kikuu ($KT_1$) kina ubebano thabiti na $KN_2$ na si kishazi tegemezi ($S_2$). Hili linaweza kuthibitika kama tutajaribu kutenganisha $KT_1$ na $KN_2$ kwa kukiweka kishazi tegemezi katikati ya viambajengo hivyo. Sentensi hiyo itakuwa kama mfano namba (6) unavyoonesha.

(6) *Juma anajua [*ingawa hakusoma sana*] mambo mengi.

Muundo wa tungo namba (6) haukubaliki katika sarufi ya Kiswahili. Kwa hiyo, sentensi hiyo ina kishazi tegemezi lakini kishazi hicho hakibebwi na kishazi kikuu cha sentensi hiyo. Kwa maneno mengine ni kishazi tegemezi lakini siyo kishazi bebwa. Muundo huo ni tofauti na ule wa sentensi (5b) kama ilivyochanganuliwa katika kielelezo tungo (3) hapa chini.




Kielelezo Na. 3: Kishazi tegemezi kinachobebwa na kishazi kikuu


Tofauti na ilivyokuwa katika kielelezo Na.2, katika kielelezo Na. 3 kuna vishazi tegemezi viwili: *"wanaolia sana"* ($S_2$) na "*kuwa nyumba inaungua*" ($KN_3$). Ingawa vishazi hivyo vyote ni tegemezi, uhusiano wake na kishazi kikuu unatofautiana. Ikumbukwe kuwa kanuni za muundo wa sentensi katika Sarufi Zalishi zinahitaji matumizi ya

viambajengo ambavyo vitaruhusu uzalishaji wa tungo sahihi tu (Chomsky, 2015). Hii ina maana kuwa ikitokea kiambajengo kimepunguzwa katika muundo wa tungo, matarajio ni tungo hiyo kutokuwa sahihi kisemantiki; yaani, tungo hiyo haitatoa taarifa inayojitosheleza.

Maelezo hayo yakitumika kutathmini ushiriki wa vishazi ($S_2$) na ($KN_3$) katika kielelezo Na.3, inabainika kwamba vyote ni vishazi tegemezi lakini kimojawapo kinaweza kuondolewa bila kuathiri uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu. Kwa mfano, tukiondoa kishazi tegemezi ($S_2$) sentensi inayobaki itasomeka: *Watoto wanasema kuwa nyumba inaungua*. Sentensi hiyo bado inatoa uarifu kamili na hivyo kishazi tegemezi ($S_2$) hakibebwi na kishazi kikuu cha sentensi kuu. Lakini tukijaribu kuondoa kishazi tegemezi ($S_3$), sentensi inayobaki itakuwa: **Watoto wanaolia sana wanasema*. Licha ya sentensi hiyo kusikika vizuri kimuundo, lakini uarifu wake si kamili. Hii ina maana kuwa kitenzi 'sema' kinahitaji taarifa zaidi ili uarifu wake uweze kukamilika. Kwa hiyo basi, kishazi tegemezi $KN_3$ ni cha lazima katika kukamilisha uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu. Kwa kifupi, kishazi hicho kimebebwa na kitenzi cha kishazi kikuu na hivyo ni kishazi tegemezi bebwa.

Aidha, kutegemeana na tabia na sifa za kitenzi cha kishazi kikuu, kuna vitenzi ambavyo uarifu wake huhitaji yambwa mbili. Tuangalie uchanganuzi wa sentensi namba (7) katika kielelezo Na.4.

(7) Juma alimwambia Ahmed kwamba Hamisi anakuja leo.




Kielelezo Na. 4: Kitenzi kinachobeba yambwa mbili


Kinachoonekana katika kielelezo Na.4ni kuwa uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu *'alimwambia'* unakamilishwa na yambwa mbili, $KN_3$ na $S_2$. Yambwa ya pili ina muundo wa kishazi tegemezi kilichobebwa ndani ya muundo wa uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu. Mabadiliko yoyote ya kuondoa mojawapo ya vijalizo hivyo yatazalisha tungo isiyokubalika katika sarufi ya Kiswahili. Sababu pekee ya kutokubalika ni kwamba kitenzi 'ambia' kisintaksia na kisemantiki hukamilisha uarifu wake kwa yambwa mbili. Jambo lingine linalobainika hapa ni kuwa kumbe hata vitenzi elekezi viko katika makundi tofauti. Vipo vinavyoweza kukamilisha uarifu wake kwa yambwa moja kama tulivyoonesha katika vilelezo Na.2 na 3. Pia kuna vitenzi ambavyo uarifu wake unakamilika panapokuwa na yambwa mbili kama inavyobainika katika sentensi (7) iliyochanganuliwa kuonesha yambwa hizo katika kielelezo Na.4.

Kwa upande mwingine, kuna nomino ambazo huhitaji ujalizi wa vishazi tegemezi ili kukamilisha uarifu wa kitenzi cha sentensi husika. Tuangalie mifano katika data (8).

(8) (a) Wazazi wake walipata taarifa *kuwa Neema amefaulu mtihani*
(b) Rose ana imani *Juma alibaki kikaoni*
(c) Habari *kwamba rais atalihutubia taifa* ziliwafurahisha wengi.

(Chanzo: Mifano ya darasani)

Katika sentensi zilizo kwenye data (8), tunaona kuwa vitenzi vyake vinahitaji yambwa moja. Hata hivyo, uarifu wa yambwa moja haukamiliki kwani nomino hizo zinahitaji ujalizi wa kishazi tegemezi ili kukamilisha uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu. Hali hii inafanana na kundi dogo la vitenzi vya lugha ya Kiingereza ambavyo Anderson (2018) anasema uarifu wake hukamilishwa na ujalizi wa kishazi tegemezi pekee. Uambajengo wa vishazi tegemezi vinavyojaliza nomino katika kielelezo tungo hautachanuza kutoka kwenye KT bali KN kama itakavyoonekana kwenye kielelezo Na.5.




Kielelezo Na.5: Kishazi kinachobebwa na nomino

Kama inavyoonekana katika kielelezo Na.5, kishazi tegemezi *'kuwa Neema amefaulu mtihani'* si yambwa kwani uambajengo wake hautoki kwenye $KT_1$ ambacho ndicho kishazi cha sentensi kuu. Kadhalika, kishazi hicho kinahusiana moja kwa moja na yambwa $KN_2$. Hata hivyo, hakitoi tu taarifa zaidi kuhusu yambwa hiyo, bali taarifa hizo zinakamilisha uarifu wa kitenzi cha sentensi kuu. Kwa hiyo, kishazi hicho si sawa na kivumishi bali ni kijalizo cha lazima katika muktadha huu kwa dhana ya kijalizo inayosisitizwa na Khamis na Kiango (2002:14) kwamba:

> "Kijalizo ni elementi muhimu na ya lazima katika sentensi ambayo kwa mujibu wa sarufi mapokeo inahusika na ukamilishaji wa taarifa muhimu za tendo linalotajwa na kitenzi cha sentensi. Kwa hali hiyo basi kijalizo ni elementi ya ujumla ambayo inajumuisha viambajengo kadhaa vya lazima vilivyo ndani ya kiarifu ukiondoa vitenzi."

Kwa ujumla, kila kundi la maneno huwa na mahitaji tofauti katika ujalizaji kutegemeana na sifa na tabia za kundi hilo la maneno katika lugha husika. Kwa mfano, Anderson (2018) anabainisha kuwa lugha ya Kiingereza ina aina ndogondogo za vitenzi kama vile vitenzi elekezi, vitenzi sielekezi pamoja na vitenzi shirikishi. Baadhi ya hizo zipo pia katika lugha ya Kiswahili (taz. Wesana-Chomi, 2017:83-84). Aidha, imedhihirika kuwa baadhi ya nomino katika

lugha ya Kiswahili huhitaji ujalizi wa kishazi ili kukamilisha uarifu wa kitenzi cha sentensi husika. Kishazi cha namna hii kinakuwa kimebebwa katika muundo wa kirai nomino lakini hadhi yake siyo sawa na ile ya kirai kivumishi ambacho ujalizi wake ni wa ziada; yaani, hata kitakapoondolewa hakitaathiri uarifu wa kitenzi.

Jambo muhimu la kujifunza hapa ni kwamba dhana ya ubebwa katika sintaksia inapaswa kuelezwa kwa umakini kwani inahusisha mambo mengi ikiwamo uziada au ulazima wa kiambajengo. Aidha, tukipanua mawanda ya kanuni ya uwekevu kama inavyoelezwa na Mgullu (1999), watumia lugha katika kuzungumza kwao huanza na vipashio vya lazima kwanza kabla ya vile vya ziada. Kwa msingi huohuo, tunapofasili dhana ya ubebwa katika sintakisia hatuna budi kutanguliza dhana shuruti kwamba viambajengo vya lazima huanza kubebana kwanza kisha kufuatwa na vile vya ziada. Hii ni sawa na yalivyo masharti ya kanuni ya ujirani wa viambajengo kama ilivyotumika kuthibitisha uziada wa kishazi tegemezi katika kielelezo Na.3.

Kwa hiyo, ni muhimu ikaeleweka kuwa ubebwa wa kishazi unaweza kuwa wa lazima au wa hiari. Kwa maneno mengine,Stockwell (1977) anaita ujirani hafifu au thabiti. Ubebwa huwa hafifu au wa hiari endapo kuondolewa kwa kiambajengo fulani hakufanyi kiambajengo kilichobaki kupoteza usarufi wake. Viambajengo vyenye ubebwa hafifu wa namna hiyo tunaweza kuviita viambajengo sibebwa. Kinyume chake, ubebwa thabiti ni ule ushikamani wa viambejengo kiasi kwamba kuondolewa kwa mojawapo ya viambajengo huathiri ukubalifu wa kisarufi wa kile kinachobaki. Kwa msingi huu, kishazi kinaweza kuwa bebwa au sibebwa kimuktadha au kutegemeana na muundo wa sentensi kuu kilimotumika kishazi hicho.

Hii inalandana na fasili ya dhana ya ubebwa katika Massamba na wenzake (1999) wanaposema kwamba ubebwa katika lugha hutokea pindi kipashio cha juu kiudarajia wa kimuundo kinapokuwa ndani ya muundo wa kipashio cha chini yake; kwa mfano, kishazi kuwa ndani ya kirai. Vilevile, inaelezwa zaidi kuwa inapotokea kishazi kikabebwa ndani ya kirai, sharti kishazi hicho kishushwe hadhi.

**Hitimisho**

Makala haya yamebaini kuwa katika sarufi ya lugha ya Kiswahili, kinachoelezwa kama kishazi bebwa hakipaswi kumithilishwa na kishazi tegemezi. Ingawa inaelezwa kuwa dhana ya kishazi tegemezi

ni ya kimapokeo kwa sababu inaangalia semantiki, madai haya hayakidhi haja kwani uainishaji wa kishazi tegemezi hauzingatii semantiki peke yake bali unahusisha na sintaksia. Hii inatokana na ukweli kuwa maneno katika lugha yana sifa na tabia tofauti kimofosintaksia na kisemantiki. Kwa hiyo, makala haya yanahitimisha kuwa kishazi tegemezi na kishazi bebwa siyo visawe bali istilahi mbili tofauti zenye kuingiliana au kuhusiana. Hii ni tofauti na mitazamo ya mwanzo iliyokuwa inazichukuliwa dhana hizi kama visawe. Mtazamo wa makala haya ni kwamba kishazi tegemezi ni aina mojawapo katika mgawanyo wa aina kuu za vishazi wakati kishazi bebwa ni miongoni mwa aina ndogondogo katika uainishaji wa vishazi tegemezi. Kama uchambuzi wa data ulivyoonesha, vishazi tegemezi vinaweza kuwa bebwa au sibebwa. Hii ni tofauti na mtazamo unaozingatia sintaksia peke yake kusema kuna vishazi vikuu na vishazi bebwa. Madai hayo ya kutumia kigezo kimoja hayakidhi uainishaji wa kategoria za kisintaksia kwa ngazi yoyote ile.

Mifano ya kutokidhi uainishaji ni mingi. Chomsky (2002, 2015) katika uundaji wa kanuni chache za kutawala miundo yote ya lugha na nadharia majumui ya lugha ni ushahidi tosha. Awali, kanuni zilizingatia sintaksia zaidi lakini baada ya kushindwa ndipo akaongeza semantiki. Vilevile uainishaji wa kategoria za kileksika katika mwanzo wake haukukidhi haja kwani ulitegemea zaidi semantiki (Rauh, 2010) lakini matokeo yanaonekana tofauti vinapoongezwa vigezo vingine vya kimofolojia na kisintaksia (Habwe na Karanja, 2004). Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa dhana ya kishazi bebwa haikidhi kuwakilisha vishazi vyote ambavyo dhima na muundo wake hutegemea kishazi kikuu.

Dhana muafaka ni kishazi tegemezi au kishazi kisaidizi kwani inajumuisha vishazi vyote visivyojitosheleza kimuundo na kimaana; yaani, haviwezi kusimama peke yake kama sentensi. Inafaa kuviita tegemezi kwa kuwa kisemantiki vishazi hivi hupata dhima yake kutegemeana na sifa na tabia za kitenzi cha kishazi kikuu. Vilevile, tunaweza kukiita kishazi kisaidizi kwani husaidia kukamilisha uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu.

Pamoja na hayo, vishazi tegemezi kutegemeana na sifa na tabia za kitenzi cha kishazi kikuu au nomino ya yambwa; huweza kuwa bebwa. Hii inatokana na vishazi tegemezi kuwa na dhima ya ujalizaji ambao unaweza kuwa shuruti au wa hiari katika

kukamilisha uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu. Kwa hiyo, ubebwa wa kishazi tegemezi ni wa kimuktadha. Tunaweza kuwa na sifa bainifu nyingi za za kishazi tegemezi lakini hatuwezi kuwa na sifa nyingi za kishazi bebwa kwani ubebwa huamuliwa na muktadha wa matumizi yake tu. Hii ina maana kuwa kishazi tegemezi fulani kinaweza kuwa bebwa katika muktadha mmoja lakini kikawa sibebwa katika muktadha mwingine.

Vishazi bebwa kwa upande wake vinaweza kufasiliwa kama vishazi tegemezi vyenye ujalizaji thabiti katika sentensi; yaani, kuwepo kwake katika sentensi hukamilisha uarifu wa kitenzi cha kishazi kikuu. Dhana hii siyo ya kupuuzwa kwani ina mchango mkubwa katika ufafanuzi wa dhana ya vishazi tegemezi. Moja ya mchango wake ni kusaidia uainishaji wa vishazi tegemezi katika makundi madogo mawili: vishazi tegemezi bebwa (vishazi bebwa) na vishazi tegemezi sibebwa (vishazi sibebwa). Vilevile, vishazi bebwa ni miongoni mwa viambajengo vinavyothibitisha kanuni ya ujirani kama inavyoelezwa na Stockwell (1977);kwamba haviwezi kutenganishwa na kishazi kikuu au huru. Kwa maneno mengine, hapawezi kuwa na kiambajengo kingine kati ya kitenzi cha sentensi kuu na kishazi bebwa. Vishazi tegemezi sibebwa kwa upande wake ni vile ambavyo kuwepo au kutokuwepo kwake hakuathiri uarifu wa kitenzi cha sentensi kuu katika muundo wake

## Marejeleo

Anderson, C. (2018). Essentials of Linguistics. Hamilton: McMaster University.

Besha, R. M. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu* (Toleo la 2). Dar es Salaam: Macmillan Aidan.

Borsley, R. (1999). *Syntactic Theory: A Unified Approach* (Toleo la 2). London: Arnold.

Chomsky, N. (2002). *Syntactic Structures* (Toleo la 2). Berlin: Mouton de Gruyter.

Chomsky, N. (2015). *Aspects of the Theory of Syntax* (Toleo la Kumbukizi ya miaka 50). Cambridge: The MIT Press.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Khamis, A. M. & Kiango, J. G. (2002). *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Kombe, L. E. (2018). Uambatishaji wa Vishazi katika Lugha ya Kiswahili: Uchunguzi wa Madai ya De Vos na Riedel (2017). *Kioo cha Lugha*, 16, 153–164.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mekacha, R. D. K. (1987). Tungo Rejeshi katika Kiswahili.*Mulika,* 19, 83–91.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mkude, D. J. (1983). Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili. Katika TUKI (Mh.). *Lugha ya Kiswahili: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I* (kur. 219–243). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mpiranya, F. (2015). *Swahili Grammar and Workbook*. New York: Routledge.

Payne, T. E. (2006). *Exploring Language Structure: A Student's Guide.* Cambridge: Cambridge University Press.

Polomé, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington, D.C.: Center for Applied Linguistics.

Rauh, G. (2010). *Syntactic Categories: Their Identification and Description in Linguistic Theories.* Oxford: Oxford University Press.

Robins, R. H. (2013). *General Linguistics: An Introductory Survey* (Toleo la 4). London: Routledge.

Stockwell, R. P. (1977). *Foundations of Syntactic Theory*. New Jersey: Englewood Cliffs.

Tallerman, M. (2011). *Understanding Syntax* (Toleo la 3). London: Hodder Education.

Wesana-Chomi, E. (1973). Towards the Syntax of Complex Sentences in Swahili.*KISWAHILI*, 42(2), 30–51.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.